



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI
UTEUZI MADIWANI WANAWAKE WA VITI MAALUM

Kwa mujibu wa Kifungu cha 86A (8) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Tume ya Taifa ya Uchaguzi katika kikao chake cha tarehe 19 Julai, Mwaka huu imewateua Madiwani wanawake wa Viti Maalum nane (8) kujaza nafasi wazi za Madiwani katika Halmashauri nane (8) za Tanzania Bara.

Uteuzi huu umefanyika baada ya kupokea taarifa kutoka kwa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa, ambaye kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 13(1) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, alitaarifu Tume ya Taifa ya Uchaguzi uwepo wa nafasi hizo wazi za Madiwani wanawake wa Viti Maalum, kupitia Chama cha Mapinduzi (CCM) na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), baada ya walioteuliwa awali kufariki dunia au kujiuzulu.

Madiwani Wanawake wa Viti Maalum walioteuliwa ni kama ifuatavyo:

NA.	JINA	CHAMA	HALMASHAURI
1.	Ndugu Ajira Rajabu Kalinga	CCM	Halmashauri ya Wilaya ya Songea
2.	Ndugu Mary Kazindogo Mbilinyi	CCM	Halmashauri ya Wilaya ya Makete
3.	Ndugu Zainab Abdi Mabrouk	CCM	Halmashauri ya Manispaa ya Kongwa

NA.	JINA	CHAMA	HALMASHAURI
4	Ndugu Restuta Aloyce Gardian	CCM	Halmashauri ya Wilaya ya Muleba
5	Ndugu Siglinda Sylvesta Ngwega	CCM	Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro
6	Ndugu Zena Saadi Luzwilo	CCM	Halmashauri ya Mji Kahama
7	Ndugu Neema Michael Massawe	CHADEMA	Halmashauri ya Wilaya ya Monduli
8	Ndugu Teodola Myula Kalungwana	CHADEMA	Halmashauri ya Manispaa ya Iringa

Imetolewa leo tarehe 20 Julai, 2018.



Jaji (Rufaa) Semistocles S. Kaijage
MWENYEKITI
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI